

# CHUO KIKUU CHA ST JOHN'S CHA TANZANIA



## KITIVO CHA HUMANITIA NA ELIMU

### JARIDA LA MNYAMPALA

### WITO WA MAKALA

**Jarida la Mnyampala (JM)** ni jarida la kitaaluma lililo chini ya Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha St John's cha Tanzania. Jarida huchapisha makala zinazohusiana na **Isimu, Fasihi na Utamaduni wa Kiswahili**.

Mhariri mkuu wa **Jarida la Mnyampala** anawakaribisha wapenzi na wataalamu wa lugha ya Kiswahili kuwasilisha makala kwa ajili ya Juzuu Na. 3 linalotarajiwa kuchapishwa mwishoni mwa mwaka 2021.

#### **Mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa makala:**

- a) landikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- b) Iwe na maneno kati ya 3000-5000, ikiwamo ikisiri isiyozidi maneno 200.
- c) Ipigwe chapa katika programu ya *word* na nafasi ya 1.5 kati ya mstari na mstari.
- d) Urejeleaji ufanywe kwa kutumia mtindo wa APA toleo la 6.
- e) Ihaririwe vizuri.
- f) Ukurasa wa kwanza wa makala ujumuishe taarifa za mwandishi kama vile jina kamili, anuani, namba ya simu, asasi au taasisi alipo n.k.
- g) **Makala zenye mwandishi zaidi ya 1 na zile zitakazoshughulikia uhusiano wa lugha ya Kiswahili na taaluma nyingine zitapewa kipaumbele.**
- h) Makala zote zitumwe kwa Mhariri Mkuu kupitia baruapepe [jaridalamnyampala@sjut.ac.tz](mailto:jaridalamnyampala@sjut.ac.tz)
- i) Tarehe ya mwisho ya kupokea makala ni **15 Mei 2021**.

Mhariri Mkuu,

Jarida la Mnyampala,

16 Machi 2021.